JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TUME YA TAIFA YA UNESCO

# Utekelezaji kazi za Tume ya Taifa ya UNESCO Zanzibar



## UNESCO

Majukumu ya UNESCO yanatekelezwa kupitia nyanja tano za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Urithi wa Dunia na Mawasiliano na Habari.



## TUME YA TAIFA YA UNESCO

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu Warsha ya mradi wa Revitalising Stone Tone of Zanzanibar Social Economic Development 25-27 Julai 2023 ambapo Waziri wa Utalii na Urithi wa Zanzibar, Simai Mohammed Said alifanya uzinduzi huo. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Oman na una lengo la kuhifadhi utamaduni pamoja na kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa miji ya kihistoria ikiwemo Mji Mkongwe ambao ni Urithi wa Dunia.

unesconatcomtz

unesco

NA MWANDISHI WETU

# Utekelezaji kazi za Tume ya Taifa ya UNESCO Zanzibar

**JAMHURI** ya Muungano wa Tanzania ni nchi mwanachama wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Kwa mujibu wa Ibara ya VII ya Katiba ya UNESCO, kila nchi mwanachama ina jukumu la kuunda Tume za Taifa za UNESCO ili kuratibu, kuhamasisha, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mikataba, makubaliano ya kimataifa na miradi ya UNESCO.

Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania (The UNESCO National Commission of the United Republic of Tanzania) ni chombo huru cha Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chenye dhamana ya kuratibu, kuhamasisha, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya UNESCO nchini ikiwa ni pamoja na mikataba ya UNESCO ambayo nchi imeridhia.

Tume ilianzishwa mwaka 1962 kupitia Waraka Na. 337 wa Baraza la Mawaziri na Mwaka 2008 ikapewa nguvu za kisheria kupitia Sheria ya Tume ya Taifa ya UNESCO, Sura ya 433.

Majukumu ya UNESCO yanatekelezwa kupitia nyanja tano za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Urithi wa Dunia na Mawasiliano na Habari.

**SEKTA YA ELIMU**

Uratibu wa Mafunzo ya Kuhamasisha Elimu ya Sayansi na Hisabati kwa Mtoto wa Kike ambapo Mwezi Machi, 2022 Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu mafunzo wezeshi kwa watumishi 41 wa sekta ya elimu kutoka Pemba na Unguja.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mheshimiwa Mhandisi Zena Said Ahmed (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Mafunzo ya Kuhamasisha Elimu ya Sayansi na Hisabati kwa Mtoto wa Kike

Mafunzo hayo yalilenga kuhamasisha elimu ya Sayansi na Hisabati kwa mtoto wa kike na kuwakumbusha wadau kuandaa mazingira wezeshi yenye kushawishi wanafunzi wasichana kupenda kujifunza masomo hayo.

Uratibu wa Mafunzo Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi Shuleni Mafunzo yalifanyika mwezi Machi 2022 katika Skuli ya Awali ya Kidutani iliyopo mjini Zanzibar. Jumla ya washiriki ilikuwa 35 iliyohusisha walimu 28 kutoka skuli za msingi 14, wadhibiti ubora wa shule 2 na maafisa 5 wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Uratibu mafunzo kwa walimu, wawezeshaji katika Vituo vya Elimu Mbadala Zanzibar Madhumuni ya jumla yalikuwa ni kutoa stadi za uwezeshaji kwa walimu wanaofundisha katika vituo vya elimu mbadala vya watu wazima.

Awali, taarifa ya mafunzo hayo ilifikishwa katika Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar.

> **UNESCO**
>
> **Majukumu ya UNESCO yanatekelezwa kupitia nyanja tano za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Urithi wa Dunia na Mawasiliano na Habari.**



Utayarishaji wa nyenzo za mafunzo ulifanywa kwa kupitia upya Sera ya Uchumi wa Bluu ya 2020 na Sera ya Elimu ya 2014.

Mada zilizoainishwa zilikuwa: Elimu Jumuishi, Stadi za Maisha; Uchumi wa Buluu na Ujasiriamali. Mafunzo ya siku tatu ya wawezeshaji yalifanyika katika vituo viwili vya kujitegemea vya Elimu Mbadala Zanzibar ambavyo ni Rahaleo (Unguja) na Wingwi (Pemba).

Mbinu ya uwezeshaji katika vituo vyote viwili ilikuwa sawa; mchakato wa mafunzo ulihusisha mawasilisho ya wawezeshaji, kazi za vikundi, mijadala ya majadiliano na mbinu ya maswali na majibu ilitumika kuakisi maudhui yaliyofunzwa kwa washiriki kabla ya dodoso ili kupata ufanisi wa mafunzo.

**SAYANSI ASILIA**

Uhamasishaji wa masomo ya sayansi kwa wadau wa elimu mkoa wa mjini magharibi unguja kuanzia tarehe 17 -19 augosti 2022.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliwajengea uwezo wadau wa elimu ili kuinua hamasa ya wanafunzi kupenda masomo ya sayansi kwa ngazi za msingi na sekondari, ambazo ni sehemu ya chini kabisa ya kuweza kuwafanya wanafunzi kupenda masomo ya sayansi kwenye ngazi za vyuo vikuu.

Sambamba na kuwajengea uwezo walimu ambao ndio wenye nafasi kubwa sana ya ushawishi wa kusoma masomo haya kwa wanafunzi wa ngazi ya msingi na sekondari, sekta ya sayansi asilia iliweza kuwajumuisha wadau wenye mamlaka za kusimamia elimu kwa ngazi za chini na kuwajengea uwezo maafisa elimu watano kutoka katika kituo cha ubunifu cha Legezamwendo na Shule ya Msingi Migombani.

**SEKTA YA UTAMADUNI**

Tume ya Taifa ya UNESCO iliandaa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mji Mkongwe mradi wa kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa utunzaji wa Urithi wa Dunia.

Mradi huo ulitekelezwa kwa shule, Asasi za Kiraia za Zanzibar Heritage Society na nyingine zinazojihusisha masuala ya utunzaji wa Urithi. Lengo la Mradi lilikuwa kuwafanya wanajamii



Katibu Mkuu WEMA na Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa UNESCO kwenye Picha ya pamoja na washiriki

# Miradi ya ushirikishwaji

kuwa sehemu ya kutunza eneo la Mji Mkongwe ambalo ni Urithi wa Dunia.

Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya UNESCO ya Dar es Salaam iliandaa kikao kilichohusisha ofisi ya Kamishna wa Utamaduni Zanzibar tarehe 10 Novemba 2021.

Lengo la kikao lilikuwa kuainisha vipaumbele katika masuala ya Utamaduni ambavyo Kamisheni ya Utamaduni ingependa UNESCO ivifanyie kazi katika mpango wa UNESCO wa mwaka 2022-2024.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika zoezi la utoaji wa Taarifa wa utekelezaji wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa 1972 mwaka 2020 yaani Third Cycle of Periodic Reporting in African Region.

Tume iliratibu upatikanaji wa taarifa za maeneo yote ya Urithi wa Dunia kwa kipindi cha miaka sita ikiwemo taarifa za Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Katika kufanukisha kazi hiyo, Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu ushiriki wa Mameneja wa Urithi wa Dunia katika Warsha ya uoanishaji wa taarifa tajwa kwa Bara zima la Afrika kwenye kikao kilichofanyika Nairobi 19-22 Februari 2020 ambapo Zanzibar ilishiriki.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu maadhimisho ya Siku ya Urithi yaliyofanyika Zanzibar tarehe 5 Mei 2020.

Katika maadhimisho hayo, washiriki kutoka maeneo mengine sita ya Urithi wa Dunia ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Mlima wa Kilimanjaro, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Pori la Akiba la Selous, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na Michoro ya Miambani ya Kondoa.

Ujumbe wa maadhimisho ulikuwa "Youth, Entrepreneurship and Heritage Sustainability in Africa".

**SEKTA MAWASILIANO NA HABARI**

Mafunzo ya kuimarisha Radio Jamii: Kuhamasisha Maudhui na Ushirikishwaji wa Wanajamii, 19 – 20 Januari 2022

Kama tunavyofahamu kumekuwepo juhudi mbalimbali katika uanzishaji, uboreshaji na uendelezaji wa vyombo vya habari vya kijamii nchini Tanzania.

Tume ya Taifa ya UNESCO kwa kushirikiana na wataalam kutoka Shule ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na ofisi ya Idara ya Maelezo Zanzibar, waliendesha mafunzo kwa waandishi wa habari 20 waliochaguliwa kutoka vyombo vya habari vya jamii vya Zanzibar juu ya kuimarisha maudhui ya vyombo vya habari vya kijamii na ushiriki wa jamii katika vipindi vya redio.

Mafunzo yalihusu maadili ya uandishi wa habari, utangazaji na kuripoti kuhusu mtazamo wa kijinsia na yaliwajengea uwezo katika kuimarisha redio jamii, kuhamasisha maudhui na ushirikishwaji wa wanajamii kwenye programu za radio.

Miradi ya ushirikishwaji

Kupitia miradi ya ushirikishwaji (Participation Programme – PP) ya UNESCO, Tume kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo Zanzibar iliandaa mafunzo kwa Maafisa Habari na Mawasiliano wa Umma na Binafsi yaliyofanyika tarehe 11 – 15 Septemba 2023 Unguja na Pemba.

Mafunzo haya yalilenga kuimarisha uwezo wa Maafisa Habari wa Umma na Binafsi na wafanyakazi wa vyombo vya habari katika kutoa taarifa za serikali kwa wananchi kwa uwazi pamoja na kufundisha umma kutumia fursa za teknolojia za sasa katika upatikanaji wa habari.

Maafisa habari na mawasiliano 40 wamejengewa uwezo katika utekelezaji wa uhuru wa kujieleza na kuendana na mabadiliko ya kidigitali katika kutangaza kazi zinazofanywa na taasisi zao.

Kuhamasisha Uhifadhi wa Nyaraka kwenye Mfumo wa Kidigiti Mwaka 2015 Mwezi Novemba UNESCO kupitia Mkutano wake Mkuu iliridhia mapendekezo ya Uhifadhi na Ufuatiliaji wa Urithi wa Nyaraka ikiwa ni pamoja na kuweka nyaraka hizo katika mfumo wa kidijiti na kuelekeza utekelezaji wake katika nchi wanachama.




**Ndugu Hassan Khatib Hassan Mkurugenzi Idara ya Habari – MAELEZO akitunuku cheti kwa mmoja ya washiriki wa mafunzo**

**MAFUNZO**

**Kupitia miradi ya ushirikishwaji (Participation Programme – PP) ya UNESCO, Tume kwa kushirikiana na Idara ya Habari Maelezo Zanzibar iliandaa mafunzo kwa Maafisa Habari na Mawasiliano wa Umma na Binafsi yaliyofanyika tarehe 11 – 15 Septemba 2023 Unguja na Pemba.**

Hivi karibuni, UNESCO iliwaomba nchi wanachama kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa kuandaa ripoti iliyohusu utambuzi, uhifadhi, upatikanaji wa jumla, hatua za kisera na ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa wa Urithi wa Nyaraka (documentary heritage).

Tume ya Taifa ya UNESCO ilishirikiana na Taasisi za Nyaraka Zanzibar kuwajengea uwezo watumishi wa Taasisi ya Nyaraka juu ya uhifadhi wa urithi wa nyaraka hizo hususani uhifadhi katika mfumo wa kidigitali na pili

**Kama tunavyofahamu kumekuwepo na juhudi mbalimbali katika uanzishaji, uboreshaji na uendelezaji wa vyombo vya habari vya kijamii nchini Tanzania.**

kukusanya na kuandaa taarifa ambayo iliwasilishwa UNESCO.

Mafunzo Kuwajengea uwezo Wanahabari, Wataalamu wa Kisheria na Wanavyuo Juu ya Haki za Kijamii na Utawala wa Kidemokrasia.

Tume ya Taifa ya UNESCO ina jukumu la kuelimisha jamii na wadau wengine juu ya haki, umuhimu wa kupata na kutoa habari katika kujenga jamii ya kidemokrasia inayofanya maamuzi kwa kuzingatia taarifa sahihi ili kuepuka madhara yatokanayo na kukosekana kwa habari.

Mji Mkongwe ni sehemu ya urithi wa Dunia na kwa kuzingatia hilo Tume ya Taifa ya UNESCO ilitembelea wakazi wa Mji Mkongwe kutoa elimu ya kuepuka ujenzi usiofaa na namna ya kujikinga dhidi ya majanga mbalimbali ikiwemo ya moto. Katika tukio hilo familia 19 walikumbwa na janga la moto.



**Washiriki wa Mafunzo ya ya kuimarisha Radio Jamii: Kuhamasisha Maudhui na Ushirikishwaji wa Wanajamii,**

unesco

# Mradi utunzaji urithi wa Dunia ulivyoinufaisha Zanzibar

>>**SMZ**, UNESCO zatekeleza mkakati kuutunza Mji Mkongwe

**NA MWANDISHI WETU**



**Timu ya UNESCO ikiwa pamoja na watalaam wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi yaZanzibar walipomtembelea Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu Zanzibar, Julai mwaka huu.**

**TUME** ya Taifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) ilitekeleza mradi uliokuwa na lengo la kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa utunzaji wa Urithi wa Dunia.

Mradi huo ulitekelezwa kwa shule, Asasi za Kiraia zinazojishughulisha na

> **Shirika la UNESCO linawajibika kwa nchi wanachama kwa kutekeleza kazi katika maeneo ya Elimu, Sayansi, Utamaduni pamoja na Habari na Mawasilisano.**

uhifadhi wa Urithi wa Dunia.

Kutokana na utekelezaji wa mradi huo, inatarajiwa kuwa utunzaji wa Urithi wa Dunia utakuwa muendelezo kwa vizazi vya sasa na vijavyo kwenye ushiriki katika kuhifadhi.

Shirika la UNESCO linawajibika kwa nchi wanachama kutekeleza kazi katika maeneo ya Elimu, Sayansi, Utamaduni, Habari na Mawasilisano.




**Moja ya picha zilizochorwa na wanafunzi wa Skuli ya Hamamni ikiwa ni sehemu ya kazi zilizofanyika wakati wa kueleimisha wanafunzi wa Sekondari**

> **UNESCO**
>
> **shauri wa Tume ya UNESCO ilijikita kwenye uzingatiaji wa taarifa za kitaalam za athari za kimazingira na Kiurithi ili kusaidia kutoa maamuzi ya utekelezaji wa mradi wowote kwenye eneo la Urithi wa Dunia.**

Katika kuhakikisha utekelezaji wa Program na bajeti ya UNESCO inafanyia kazi mambo ambayo yatakuwa kwa maslahi ya Taifa.

Tume ya Taifa ya UNESCO katika sekta ya Utamaduni ilifanya kikao kilichohusisha ofisi ya Kamishna wa Utamaduni Zanzibar tarehe 10 Novemba 2021. Kikao kiliainisha vipaumbele katika masuala ya utamaduni ambavyo Kamisheni ya Utamaduni ingependa UNESCO ivifanyie kazi katika mpango wa UNESCO wa mwaka 2022-2024.

Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika zoezi la utoaji Taarifa kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa 1972 mwaka 2020 yaani Third Cycle of Periodic Reporting in African Region.

Tume iliratibu upatikanaji wa taarifa za maeneo yote ya Urithi wa Dunia kwa kipindi cha miaka sita ikiwemo taarifa za Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu maadhimisho ya Siku ya Urithi yaliyofanyika Zanzibar tarehe 5 Mei 2020.

Katika maadhimisho hayo, yalihusisha washiriki kutoka maeneo mengine sita ya Urithi wa Dunia ambayo ni Hifadhi ya Taifa ta Serengeti, Hifadhi ya Mlima wa Kilimanjaro, Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Pori la Akiba la Selous, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara na Michoro ya Miambani ya Kondoa.

Ujumbe wa maadhimisho ulikuwa " Youth, Entrepreneurship and Heritage Sustainability in Africa".

Kufuatia tukio la kuzuka kwa moto siku ya 30 Agosti 2022 katika eneo la Kiponda ndani ya Mji Mkongwe ambao ni eneo la Urithi Dunia, Tume ya Taifa ya UNESCO ilituma taarifa UNESCO kwenye kituo cha Urithi wa Dunia. Tume pia ilishiriki kwa kuchangia waathirika

unesco

# Mradi utunzaji urithi wa Dunia ulivyoinufaisha Zanzibar

wa tukio hilo.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu Warsha ya mradi wa Revitalizing Stone Tone of Zanzibar Social Economic Development 25-27 Julai 2023 ambapo Waziri wa Utalii na Urithi wa Zanzibar, Simai Mohammed Said alifanya uzinduzi huo.

Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Oman na una lengo la kuhifadhi utamaduni pamoja na kuimarisha uhifadhi na usimamizi wa miji ya kihistoria ikiwemo Mji Mkongwe ambao ni Urithi wa Dunia.

Mji Mkongwe wa Zanzibar umekuwa na changamoto nyingi za kiuhifadhi zinazotokana na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo pamoja na uchakavu wa majengo yake.

Hali hiyo inatishia kuathiri utunzwaji wa sifa mahsusi zilizoingiza Mji Mkongwe kwenye Urithi wa Dunia.

Tume ya Taifa ya UNESCO katika nafasi yake ya kutoa ushauri (Advisory capacity) ilishiriki kwenye kikao kilichoitishwa na Kituo cha Urithi wa Dunia kikihusisha Mamlaka ya Mji Mkongwe, Wizara ya Utalii na Urithi Zanzibar, tarehe 15 hadi 18 Januari 2023 ili kufafanua umuhimu wa miradi ya maendeleo katika eneo la Mji Mkongwe inayozingatia utunzwaji na uhifadhi wa Urithi wa Dunia.

Ushauri wa Tume ya UNESCO ulijikita kwenye uzingatiaji wa taarifa za kitaalam za athari za kimazingira na Kiurithi ili kusaidia kutoa maamuzi ya utekelezaji wa mradi




wowote kwenye eneo la Urithi wa Dunia.

Tume ya Taifa ya UNESCO inaratibu utekelezaji wa Mikataba ya UNESCO ikiwemo Mkataba wa Utamaduni wa UNESCO wa 2005. Uandaaji wa ripoti hii ulishirikisha Wizara na taasisi za Serikali na kiraia kutoka pande zote mbili za Muungano.

Kwa upande wa Zanzibar, Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo ya Zanzibar pamoja na idara ya Sanaa na Filamu zilishiriki katika uandaaji wa Ripoti ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa UNESCO wa 2005, kazi hiyo ilianza mwishoni 2019 na kuendelea hadi mwanzoni mwa mwaka 2020.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliwasilisha kazi hiyo UNESCO makao makuu mwishoni mwa mwezi Februari 2020.

UNESCO hufanya tathmini ya hali ya uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia. Tathmini hiyo hufanywa baada ya vikao vya Kamati ya Urithi wa Dunia kufanya maamuzi iwapo kuna viashiria vinavyoonekana vinaweza kuathiri sifa mahsusi za eneo husika.

Kutokana na kuwepo kwa mipango na utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo ndani ya eneo la Mji Mkongwe ambao ni eneo la Urithi wa Dunia, UNESCO iliomba kuja kufanya tathmini hiyo.

Tume ya Taifa ya UNESCO iliratibu ziara ya watalaam hao iliyofanyika Julai 2023. Timu hiyo ilipata fursa ya kumtembelea Mh. Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi ambapo alieleza dhamira ya serikali yake kuendelea kuuhifadhi Mji Mkongwe.

**Tume ya Taifa ya UNESCO katika nafasi yake ya kutoa ushauri (Advisory capacity) ilishiriki kwenye kikao kilichoitishwa na Kituo cha Urithi wa Dunia kikihusisha Mamlaka ya Mji Mkongwe, Wizara ya Utalii na Urithi Zanzibar, tarehe 15 hadi 18 Januari 2023 ili kufafanua umihimu wa miradi ya maendeleo katika eneo la Mji Mkongwe unazozingatia utunzwaji na uhifadhi wa Urithi wa Dunia.**